## Kusoma Zaidi

# Sababu za maenezi ya Kiswahili katika Afrika Mashariki na Kati kabla ya uhuru.

Kuna sababu kadhaa zilizochangia kuenea kwa lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki na Kati. Sababu hizo ni pamoja na utawala, biashara, dini, matokeo ya vita vya dunia na harakati za ukombozi/harakati za kisiasa.

- **Kuwepo kwa Wajerumani na Waingereza** Afrika Mashariki na Kati. Makundi haya yalitumia lugha ya Kiswahili kutekeleza sera zao. Katika shughuli zao za kibiashara walitumia Kiswahili. Walitumia lugha hii kuwagawanya na kuwatawala Afrika. Mambo haya yalichangia kuenea sana kwa Kiswahili.

- **Biashara.** Kulikuwa na makundi mawili makuu ya kibiashara: Waafrika wa pwani walioshirikiana na wenzao wa bara, na Waarabu pamoja na Wafrika waliobobea katika biashara ya pembe za ndovu na watumwa. Kiswahili kilitumiwa sana katika biashara hii.

- **Dini.** Dini ya Kikristo na Kiisilamu ni mojawapo ya asasi ambazo zilitoa mchango mkubwa kueneza Kiswahili. Tafsiri za vitabu vya dini ilifanywa kwa lugha ya Kiswahili ili kueneza dini miongoni mwa wananchi.

- **Wakati wa vita vya dunia**, Wajerumani na Waingereza walipigana wakiwa katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, na baada ya Wajerumani kushindwa na Waingereza walitumia Kiswahili kuwatawala Wafrika.

- **Nia ya kujikomboa kutokana na ukoloni.** Baada ya Waafrika kuchoshwa na utawala mbaya wa ukoloni, walianza harakati za kuwashawishi Waafrika wenzao kushirikiana ili waweze **kujikomboa kutoka mikononi mwa wakoloni.** Hivyo walikitumia Kiswahili sana kuwasiliana ili wajikomboe.

Hizi ni miongoni mwa sababu ambazo zilichangia katika kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika eneo hili la Afrika Mashariki na Kati kabla ya uhuru.